TANGAZO LA SERIKALI NA. 708 la tarehe 02/12/2022

SHERIA YA MIPANGOMIJI,

(SURA YA 355)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1))*

AMRI YA KUPANGA ENEO LA KILOLELI YA MWAKA, 2022

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kupanga Eneo la Kiloleli ya Mwaka, 2022.

Kutangazwa kwa eneo la upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpango wa jumla na kina wa eneo

3. Mpango wa jumla na wa kina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge.

## JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la Upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatayo:

"Unaanzia katika alama ya mpaka K1 kwenye makutano ya barabara ya Sikonge na Shule ya Sekondari ya Langwa yenye majira-nukta 495499E, 9350795N; baada ya hapo mpaka utaelekea Kusini - Mashariki katika uelekeo wa S93$^{0}$6'12"E kwa umbali wa kilomita 0.7 hadi alama ya mpaka K2 iliyopo katika makutano ya barabara ya Sikonge na Wakulima kwenye majira-nukta 495765E, 9350094N; baada ya hapo mpaka utaelekea Mashariki - Kusini katika uelekeo wa E120$^{0}$8'0"S kwa umbali wa kilomita 2.08 hadi alama ya mpaka K3 iliyopo barabara ya Mbugani yenye majira-nukta 497852E, 9348738S; baada ya hapo mpaka utaelekea Mashariki - Kaskazini katika uelekeo wa E148$^{0}$9'52:N kwa umbali wa kilomita 0.8 hadi katika alama ya mpaka K4 iliyopo barabara ya Kanyamsenga yenye majira-nukta 498637E, 9349137N; baada ya hapo mpaka utaelekea Kaskazini - Mashariki katika uelekeo wa N109$^{0}$7'16"E kwa umbali wa kilomita 1.3 hadi alama ya mpaka K5 iliyopo barabara ya Kipili yenye majira-nukta 498985E, 9350484N; baada ya hapo mpaka

*Tangazo la serikali na. 708 (linaendelea)*

utaelekea Magharibi - Kaskazini katika uelekeo wa W88$^0$5’52”N kwa umbali wa kilomita 1.3 hadi alama ya mpaka K6 iliyopo bonde la mpunga Kaskazini mwa makazi ya Kiloleli katika majira-nukta 497732E, 9350826N; baada ya hapo mpaka utaelekea Magharibi katika uelekeo wa W112$^0$7’28”kwa umbali wa kilomita 2.2 hadi ulipoanzia”

Dodoma,
8 Novemba, 2022

ANGELINE S. MABULA
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na*
*Maendeleo ya Makazi*